**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 29 Septemba, 2023**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

111. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Moja ya malengo ya kuwepo mashirikiano baina ya Serikali yetu na Serikali mbali mbali duniani ni pamoja na kuongeza ufanisi wa Serikali yetu na kuipunguzia mzigo wa kiuchumi.

(a) Je, lengo hili limefuatiliwa kwa kiasi gani.

(b) Je, Serikali inaweza kusema kwa kiasi gani imefikia malengo ya mashirikiano hayo.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

11. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Wanasheria ni kama wataalamu wengine wanatakiwa kila baada ya muda waende wakasome ili kuongeza ujuzi na hatimae waweze kufanya kazi kwa umakini na ufanisi zaidi.

(a) Ni vipi Wanasheria wa Zanzibar wanapatiwa fursa hizo.

(b) Je, kuna mpango gani endelevu na wa makusudi wa kuwapeleka Wanasheria hao masomoni.

60. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Walimu wa Madrasa wamekuwa na mchango mkubwa katika kuilea jamii na kujenga taifa la watu wazalendo na wenye khofu ya Mungu.

(a) Je, Ofisi ya Mufti inawashirikisha vipi walimu wa Madrasa zetu katika jimbo la Mwanakwerekwe na majimbo mengine kupata stahiki mbali mbali zikiwa ni kama motisha ya utendaji wa kazi zao za kujitolea.

(b) Ni kwa vipi walimu hawa wanapata semina na makongamano mbali mbali kama walimu wengine wa kawaida.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

14. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunakipongeza Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa kuwa na kiwanda cha kutengenezea faiba na boti za aina mbali mbali kwa ajili ya kuuza. Hata hivyo, imebainika kuwa kasi ya ununuzi na idadi ya wateja wa kuzinunua boti hizo ni ndogo sana.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa KMKM inapata wateja wa kuzinunua faiba na boti wanazozitengeneza.

(b) Kwa nini Serikali isiihakikishie KMKM kuwa faiba wanazozitengeneza zitanunuliwa na wavuvi wa Zanzibar, ili kuongeza kipato na kukiinua kiwanda chao.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

92. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa mujibu wa vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna taarifa kwamba mgao wa Zanzibar kutokana na pesa za gawio la Muungano kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) umeongezeka kutoka asilimia 4.5 ambayo tulikuwa tumeizowea hapo zamani na kuwa asilimia 9 kwa sasa.

(a) Kupitia mgao huo wa sasa, Zanzibar imeshapata gawio la kiasi gani na kwa kipindi gani.

(b) Kutokana na mabadiliko hayo ya mgao, utekelezaji wake umeanzia lini kwa Zanzibar.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

39. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Je, ni tafiti ngapi za mbegu za mazao ya kilimo zimefanyika hivi karibuni na kuleta matokeo chanya.

40. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Je, ni lini Wizara itajikita katika kutoa elimu ya mbegu kwa wakulima wetu ili kuondokana na mazao ya miongo.

**Wizara ya Afya:**

64. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Pamoja na juhudi kubwa za kuimarisha huduma za afya nchini mwetu, Serikali yetu imefanya vizuri katika ujenzi wa majengo mbali mbali ya afya, lakini inafahamika wazi kuwa, bado tunakabiliwa na changamoto mbali mbali za vifaa tiba katika majengo hayo ya hospitali.

    (a) Je, ni vipimo vipi ambavyo vinakosekana sana katika hospitali za Serikali.

    (b) Je, Wizara yako inategemea vipimo hivyo vitaletwa lini na kutumika katika hospitali zetu.

<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>

106. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kuwa kumekuwa na upungufu mkubwa wa kusafirisha zao la karafuu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo thamani halisi ilipunguwa na kuwa 149.2 bilioni sawa na tani 3,958.5 zenye thamani ya USD 32.2 bilioni, tofauti na mwaka 2021/2022 ambapo thamani halisi iliongezeka na kuwa Tzs 206.0 bilioni sawa na tani 8,321.6 zenye thamani ya USD 60.5.

(a) Kwanini usafirishaji wa karafuu umepungua kwa kiasi hicho kwa mwaka 2022/2023 ukilinganisha na mwaka 2021/2022.

(b) Je, Wizara imefanya tafiti ngapi za kuimarisha na kujua sababu za kupungua zao la karafuu.

(c) Kwa kuwa karafuu ni miongoni mwa zao kuu la biashara, je Wizara ina mkakati gani wa kuimarisha zao hili.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

96. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Dimani) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi karibuni kumeripotiwa matukio mengi ya ajali mbaya kwa watoto wanaopakiwa kwenye vyombo vidogo vya moto vya maringi mawili maarufu kama “Clicks” na kuwasababishia vifo na majeruhi.

(a) Je, Serikali haioni sasa kuwa muda umefika wa kupiga marufuku kabisa upakiaji wa watoto kwenye vyombo vya “Clicks” ambavyo havipo salama.

(b) Katika kuwalinda watoto na ajali, kwanini hatua kali za kisheria zisichukuliwe kudhibiti upakiaji wa watoto kwa mtungo (mshikaki) kwenye vyombo vyote vya moto vya maringi mawili.

99. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani)
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa muda mrefu sasa kumeonekana matukio ya baadhi ya madereva hasa vijana kuendesha gari kwa fujo, kelele na misererko (drifting) kwenye mizunguko ya barabara (round about) na kuleta kero za kelele, taharuki na kuhatarisha usalama wa watumiaji wengine wa barabara.

(a) Serikali kwa kushirikiana na jeshi la Polisi la Usalama Barabarani, wanachukua hatua gani endelevu kudhibiti matukio hayo.

(b) Kwa kuwa baadhi ya madereva vijana wanaofanya vitendo hivyo wanajirekodi na kurusha kwenye mitandao na kwa kuwa zipo kamera za CCTV zinachukuwa matukio hayo, kwanini Jeshi la Polisi haliwafungulii mashtaka na kuwachukuliwa hatua za kisheria madereva hao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**29 Septemba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**